**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TECHNOLOJIA**
**OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**
**SHULE YA SEKONDARI KIVINJE**

Simu. Na: 0786505676
Kumb: Na. KVSS/A.5/VOL.1/009 TAREHE **……………………**

**MWANAFUNZI …………………………………….**
**…………………………………………………………..**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIVINJE KIDATO CHA KWANZA MWAKA**

## 1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukualifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020 shule ya sekondari Kivinje ipo umbaliwa wa km 3 kutoka stendi kuu ya magari ya Kivinje (Mtaa wa DDC standi).

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 06.01.2020 na mwisho wa kuripoti tarehe 13.01.2020 ndani ya siku saba.

Ukumbuke kwamba wewe umebahatika sana kupata nafasi hii, muhimu ambayo umepewa na Taifa. Unatakiwa uweke juhudi kubwa sana katika masomo, kazi, michezo pamoja na mwenendo bora wa tabia kwa manufaa yako na taifa Lako. Aidha inakubidi kufuata sheria na kanuni zote za shule. unatakiwa utumie vizuri nafasi hii uliyopewa na serikali kusoma masomo unayotakiwa kusoma kwa lazima , kidato cha kwanza ni masomo Tisa (9).

i. Civics
ii. History
iii. Geography
iv. Kiswahili
v. English
vi. Physics
vii. Biology
viii. Chemistry
ix. Basic mathematics

Shule itafunguliwa tarehe 06/01/2020 unatakiwa kufika siku hiyo bila kukosa kwa ajili ya kuanza masomo. Unatakiwa kuripoti ndani ya siku saba toka shule ifunguliwe. Fika na mzazi au mlezi unayemtegemea ili atambuliwe na shule.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Unatakiwa uzingatie maagizo yafuatayo ili uweze kujiunga na shule hii.

**2.1 SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORM)**
Unatakiwa uwe na sare ilio sahihi na inayokubaliwa na uongozi wa shule. Mara nyingi wanafunzi wanaleta sare isiyo sahihi inayo fanana na wewe (Inayobana) ukileta aina hiyo haitakubaliwa.

**A. WAVULANA**
- Suruali mbili za Ton Red (Damu ya Mzee) Mshono wa Linda Jeans Stail haitakubaliwa na vile vile suruali za modo hazitakubaliwa , mkanda wa ngozi rangi nyeusi.
- Mashati mawili meupe mikono mifupi ( yasiwe ya kubana )
- Viatu vyeusi jozi mbili
- Soksi nyeusi jozi mbili.

**B. WASICHANA.**
- Sketi mbili rangi ya Ton Red (Damu ya mzee) Linda Box na zifike kwenye kifundo cha mguu.
- Mashati/ blauzi mbili nyeupe zenye mikono mirefu nusu kanzu. kwa wanafunzi waislamu na wakristo mikono mifupi.
- Viatu vyeusi jozi mbili
- Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
- Kwa wanafunzi waislamu wanaruhusiwa kuvaa hijabu nyeupe ya kawaida isiyo na Mapambo. Hijabu hiyo iwe ya duara pia iwe ndefu.

**NB:-**
- Suruali iwe na pindo na tanapu pia iwe pana saizi ya vipimo 20
- Viatu na soksi visiwe vya rangi, madoa, mistari wala mapambo ya aina yeyote pia viatu visiwe vya kupanda (ngazi) wala mabuti na bajaji.
- Hauruhusiwi kuvaa kofia, kandambili mapambo ya aina yeyote ile kama bangili. Kufu, pete, heleni n.k vilevile wanafunzi wakike wanaruhusiwa kusuka nywele zisizopungua 5 na zisizo zidi 7 mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara bila sababu inayokubalika na utamaduni wa kiafrika au bila ruhusa maalumu.
- Vitambaa vya sare ya shule vimeambatanishwa kwenye barua hii hivyo unatakiwa kupata kitambaa kilicho sahihi sio “kinachofanana”

**C. SARE ZA MICHEZO**

**I. WASICHANA**
- Tisheti moja rangi ya blue
- Raba nyeupe kwa ajili ya Michezo

**II. WAVULANA**
- Tisheti moja rangi ya blue
- Bukta moja rangi ya blue
- Raba nyeupe kwa ajili ya Michezo.

**D. MAHITAJI KWA AJILI YA USAFI NA MASOMO**
- Aje na ufagio mmoja wa Mti
- Aje na daftari tisa (9)
- Aje na kalamu na mkebe wa hesabu
- Aje na begi kwa ajili ya kubebea daftari

**E. AFYA**

Kabla ya kufika shule unatakiwa kupima afya yako na mganga wa serikali na kujaza kikamilifu fomu iliyoamabatanishwa.

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria NA. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu sayansi na technologia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa Mwili mavazi na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i. Kutunza mali za umma.

### 3.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a. Wizi
b. Uasherati na ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e. Kupigana au kupiga
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g. Kudharau Bendera ya Taifa
h. Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i. Kutoa mimba.
j. Kuoa au kuolewa
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l. Kukataa adhabu kwa amakusudi
m. Kuwa na simu ya mkonononi

**3.2: MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

a. Medical Examintaion form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya serikari. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

b. Nakala ya cheti cha kuzaliwa itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

c. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi.

d. Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

4.0: Tafadhali somo kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**……………………………….**
**MKUU WA SHULE**
**KIVINJE SEKONDARI.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION OF SCIENCES AND TECHNOLOGY**

KIVINJE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 36,
**KILWA MASOKO.**
Date ……………………

Ref. No. …………………………

The Medical Officer
………………………………….
…………………………………
…………………………………

**REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS …………………………………………**

Please examination the above named pupil and give us a report regarding his/ her suitable for secondary school studies.

1. **Pupil's full Name ………………………………………………………………………**
2. Blood **……………………………………………………………………..……………**
3. **Stool ……………………………………………………………………..……….**
4. **T.B.Test ………………………………………………………………………………**
5. **Syphilis test ……………………………………………………………….……..**
6. **Urine examination ………………………………………………..………..……**
7. **Eye test ………………………………………………………………………………**
8. **Chest …………………………………………………………………………..…**
9. **Ears ……………………………………………………………………..…………..**
10. **Spleen ……………………………………………………………………………..**
11. **Abdomen ……………………………………………………………..…………..**
12. **Pregnancy (Girls only) ……………………………………………………………….**

I certify that the above pupil is suitable/ unsuitable for studies

If unsuitable please give reasons

**……………………………………………………………………………………………….**

**……………………………………………………………………………………………….**

**……………………………………………………………………..……..……………………..**

Name of Medical Officer **…………………………………………………..………..……………**

**Signature of Medical Officer ……………………………………..………………………**

**Date ……………………………………………………………………………………….**

**Official stamp ………………………………………………………………………….**

# UTHIBITISHO WA MZAZI

Mimi ……………………..………………………………………………………………………

Ninakubali mtoto wangu ……………………………………………………………………….

Asome katika shule ya Sekondari kivinje. ninahakikisha kwamba wakati wote mwanangu atakapokuwa anasoma hapo shule.

a. Atakuwa hana ruhusa ya kwenda katika majumba ya wageni maeneo ya ulevi, utamaduni n.k.

b. Ninaahidi kumpatia vifaa vyote vinavyohitajika shuleni ikiwa ni pamoja na chakula. Mahali pa kulala wakati wote mpaka amalize masomo yake. Na kwamba sita omba uhamisho katika kipindi chote atakachosoma hapa shuleni.

c., Ninaahidi kuwa nitahakikisha anafuata sheria zote za shule, pale atakaposhindwa hatua ipasavyo ichukuliwe dhidi yake.

d. Ninaahidi kumlete shuleni kwa wakati uliopagwa bila ya kumchelewesha ili nafasi yake isichukuliwe na wanafunzi wengine.

e. Mwanangu akiwa shuleni alelewe katika dini ya ……………………………………..….

f. Anuani yangu ni ………………………………………………………………….….
…..……………………………………………………………………....
……………………………………………………..……………...

g. Sahihi yangu mimi mazazi/mlezi ………………..…………………………………..……
Tarehe ……………………………………………………………….

h. Sahihi yangu mtoto …………………………………………………………………..….
Tarehe ………………………………...…………………………..…

i. Namba ya simu ya mzazi …………………………………………………………………

**NB:-** Kumbuka kuwa muda wa kuripoti shuleni ni saa 1:00 asubuhi na vipindi vya masomo vinaanza saa 2:00 asubuhi. Hivyo basi mzazi unapaswa kuhakikisha kuwa mwanao anawahi shuleni kama ratiba ya shule inavyoelekeza.